

Desimali Kisimani

kujumlisha na kutoa desimali



Age
Umri
7+



Siku moja Kiduchu, Koba, Kibena
na Baraka walikuwa wanacheza mpira.



Koba alipiga mpira kwa nguvu kuelekea golini.



Mpira ukaruka juu na kuvuka goli.
Ulidondokea nje ya ukuta nyumbani kwa Mzee Kigo.



“Aah, jamani!” Koba alisema.



Koba na Kiduchu walibishana
kuhusu nani aende kuufuatilia mpira.




Kibena alishauri waende wote
kufuatilia mpira nyumbani kwa Mzee Kigo.



Kiduchu alikumbuka kugonga geti vizuri.



Mzee Kigo alitoka na kuwauliza wanataka nini.



Hamna aliyeweza kusema wanataka nini.
Hatimaye Kibena alivunja ukimya na kumuuliza
Mzee Kigo kama ameona mpira wao.



Mzee Kigo aliwaambia kuwa hajaona mpira
maana alikuwa ndani. Aliwakaribisha kwake ili
watafute mpira.




Watoto walitafuta mpira kila mahali.



Kiduchu na Koba walitafuta
mpira ndani ya mapipa.



Baraka ndiye aliyeuona mpira kisimani.



Watoto walichungulia
na kuona kisima kirefu
sana. Koba alishauri
watafute kamba ya
kuvutia mpira kisimani.




Mzee Kigo alikuwa na kamba moja tu na ilikuwa fupi sana. Akawaambia kamba yake haitatosha. Maana kisima ni kirefu sana mita tano nukta nane.



Aliwapa watoto futi ya kupimia urefu na kuwaambia watumie ubongo kutafuta njia ya kupata mpira wao.



Wakapima ile kamba ya Mzee Kigo kwa kutumia futi ya kupimia. Ile kamba ilifika kwenye sentimeta themanini au mita sifuri nukta nane.




Kibena alifanya hesabu za haraka haraka kichwani na kusema wangehitaji kamba yenye urefu wa mita tano. Baraka alishangaa sana akamuuliza Kibena amefanyaje.


$$\begin{array}{r} 5.8 \\ - 0.8 \\ \hline 5.0 \\ \hline \hline \end{array}$$



Kibena akamwonyesha Baraka, “Mzee Kigo amesema kisima kina urefu wa mita tano nukta nane. Na kamba yake ina urefu wa mita sifuri nukta nane.




$$\begin{array}{r} 5.8 \\ - 0.8 \\ \hline \end{array}$$

Kwa hiyo nimechukua urefu wa kisima toa urefu wa kamba. Angalia nilivyohakikisha desimali zimejipanga pamoja kwenye mstari.





$$\begin{array}{r} 5.8 \\ - 0.8 \\ \hline 0 \end{array}$$

Nane toa nane
ni sifuri.

Na hii **nukta** unaishusha kama ilivyo.

Tano toa sifuri ni ngapi, Baraka?”

“Tano,” Baraka alijibu.

$$\begin{array}{r} 5.8 \\ - 0.8 \\ \hline 5.0 \end{array}$$

“Hivi ndivyo nilivyojua tunahitaji kamba ya urefu wa mita tano,” Kibena alisema.


Watoto walikubaliana kutafuta kamba nyingi zaidi.
Walikimbia haraka kuelekea sehemu mbalimbali.




Kibena alielekea mjini, njiani alikutana na muuzaji
matunda na kumuuliza kama ana kamba.
Hakuwa nayo.




Koba alienda ufukweni kuomba kamba kutoka kwa wavuvi, lakini alikuta wavuvi wote wamelala.






Kiduchu alienda nyumbani kwake.



Aliona mkanda wa suruali mezani na kuuchukua.



Akachukua waya wa TV!




Baraka alienda msituni, akiwa msituni alisikia mtu
akiimba, “Hisabati ni nini?
Hisabati mikakati, kila siku na kila wakati.”
Aliifuata hiyo sauti msituni.



Wakati huo Kibena na Koba walikuwa wamesharudi kisimani. Kibena alikuwa ameleta kipande cha kamba nyeusi.




Koba hakupata kamba.
Hivyo aliamua kutoa kamba za viatu vyake.




Kamba za viatu vyake zilikuwa na urefu wa mita
sifuri nukta tisa.



0.9 m



Kupata urefu wa kamba zote mbili, alikokotoa
sifuri nukta tisa jumlisha sifuri nukta tisa.




$$\begin{array}{r} 0.9 \\ + 0.9 \\ \hline \end{array}$$




$$\begin{array}{r} 0.9 \\ + 0.9 \\ \hline 1.8 \end{array}$$

“Tisa jumlisha tisa
ni kumi na nane.
Naandika nane hapa,
hii moja naibeba.”

Kibena alimkumbusha kushusha ile **nukta**.



$$\begin{array}{r} 0.9 \\ + 0.9 \\ \hline 8 \end{array}$$

A red arrow points down from the decimal point in the second number (0.9) to a cyan dot placed below the horizontal line, indicating the correct placement of the decimal point in the result.

Koba aliendelea,
“Sifuri jumlisha sifuri...
ni sifuri, na ukiongeza
na ile moja tuliyoibeba...

tunapata moja nukta
nane. Kamba zote mbili
zina urefu wa mita moja
nukta nane!

Dah bado! Tuongeze na
ya kwako, Kibena!”


$$\begin{array}{r} 0^1.9 \\ + 0.9 \\ \hline 1.8 \end{array}$$

Wakapima kamba nyeusi ya Kibena.
Ilikuwa na urefu wa mita moja nukta tatu.

1.3 m



Kibena akafanya moja nukta
tatu jumlisha moja nukta nane.



$$\begin{array}{r} 1.3 \\ + 1.8 \\ \hline 3.1 \end{array}$$

“Tatu jumlisha nane ni kumi na moja.
Naweka moja hapa nashusha nukta
kisha nabeba moja.


Moja jumlisha moja ni mbili,
jumlisha na ile moja tuliyoibeba
tunapata tatu. Jumla ni urefu
wa tatu nukta moja.”

“Msijali, nimeleta kamba nyingine hapa!”
alisema Kiduchu, akionyesha waya wa TV na mkanda.




Aliendelea kusema, “Nimeshapima kamba zangu.
Mkanda una urefu wa mita sifuri nukta saba...

0. 7m



na waya una urefu wa mita moja nukta mbili.”



“Poa, Kiduchu!”
alisema Kibena.
“Tutajumlisha hii
tatu nukta moja ya
kamba yangu na
kamba za Koba,
mkanda wa Kiduchu,
(mita sifuri nukta moja)
na **waya wa TV**
(mita moja nukta mbili).”

$$\begin{array}{r} 3.1 \\ + 0.7 \\ 1.2 \\ \hline \end{array}$$

“Ngoja nijumlishe,” alisema Kiduchu.


“Moja jumlisha saba jumlisha mbili ni kumi. Naandika sifuri, nabeba moja halafu nashusha ile nukta.

$$\begin{array}{r} \textcircled{1} \\ 3.1 \\ + 0.7 \\ 1.2 \\ \hline .0 \end{array}$$

Tatu jumlisha sifuri jumlisha moja, jumlisha moja tuliyoibeba ni tano.”

“Heh, tumepata tano kamili,”
Kibena alisema.


$$\begin{array}{r} \textcircled{1} \\ 3.1 \\ + 0.7 \\ 1.2 \\ \hline 5.0 \\ \hline \hline \end{array}$$




“Tukiongeza hizi mita tano na ile kamba ya Mzee Kigo yenye urefu wa mita sifuri nukta nane, tunapata mita tano nukta nane, sawasawa na urefu wa kisima, jamani!”
Kiduchu alisema.

$$\begin{array}{r} 5.0 \\ + 0.8 \\ \hline 5.8 \\ \hline \hline \end{array}$$

Watoto walifunga kamba zote pamoja:
kamba, mkanda, waya wa TV na kamba za viatu.



Wakaifunga na ndoo mwishoni.



Wakawa wanaimba huku wakitoa mpira:

“Msichana mdogo,
amekaa pembeni ya kisima analia!
Analia nini?
Anataka mpira!
Mpira uko wapi?
Uko ndani ya kisima.
Tumia ubongo! Tumia ubongo!
Utapata mpira wako.
Tumia ubongo! Tumia ubongo!
Mpaka upate mpira.”



Walishusha ndoo kisimani,
kamba yote ikaingia kisimani
wakaacha sehemu ndogo tu
ya kushika.





Wakachungulia kisimani
na kuona kuwa ndoo
haikufika chini yalipo
maji na mpira.

“Kwa nini haijafika?”
Kiduchu alisema kwa
mshangao.



“Sielewi!
Tumeweza kupata
kamba yenye urefu wa
mita tano nukta nane
jumlisha ndoo,
haitoshi?”
Koba aliuliza.

Ghafla kichwa cha twiga
kikatokea kwenye maji.



Watoto wakaangalia juu kwa mshangao na kumwona Anko T na Baraka. Baraka akasema, “Sijapata kamba lakini nimeleta rafiki kutoka msituni!”




“Karibu Anko T,” alisema Kibena. “Unaweza kutusaidia? Tunataka kutoa mpira kisimani. Kisima kina urefu wa mita tano nukta nane. Hii kamba tuliyoiumunganisha ina urefu wa mita tano nukta nane! Lakini haifiki chini, sijui kwa nini?”



“Mlipima vipande vyenu kabla ya
kuvifunga pamoja?”

“Ndiyo,” watoto walijibu.



“Angalia vifundo vyote hivi.
Hamuoni kama vimechukua
urefu wa kamba!” alisema Anko T.



Watoto walicheka na kusema,
“Ndiyo maana haitoshi!
Anko T una akili sana!”




Anko T akawaambia anajua kitu
kirefu sana wanachoweza kutumia.
Watoto wakaangaliana kwa muda.



“Mmh... kitu kirefu...kirefu sana,
kama shingo yako, Anko T?”

“Vizuri sana, Baraka. Umepatia,” Anko T alimjibu.



Kiduchu akapima shingo ya Anko T kwa kutumia futi ya kupimia. Shingo yake ilikuwa ndefu kuliko hata hiyo futi.



Anko T akashika mshikio wa ndoo kwa kutumia
meno yake na kushusha kichwa chake kisimani.




Akapandisha ndoo juu.
Kiduchu akachukua mpira toka kwenye ndoo.



Kila mmoja alishangaa, kuona Da Chura akiruka toka kwenye ndoo. Watoto walicheka na kukimbia kuelekea uwanja wa mpira.




Anko T alijitolea kuwa refa.
Alipuliza filimbi na mchezo ukaanza.



Baraka akapiga mpira.



Mpira ukaruka juu na kuvuka ukuta ukaishia
kudumbukia kwenye kisima tena!





Mwisho

Imeandaliwa na

ubongo.co

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa njia
ya aina yoyote bila idhini ya mwandishi,
UBONGO INTERNATIONAL.